

Je, ni SAWA kuchanganya chanjo za COVID-19?

Ni muhimu sana kupokea dozi 2 za chanjo za COVID-19 ili upate chanjo kamili dhidi ya COVID-19 na aina zake nyingine. Utatimiza mahitaji ya chanjo kamili wiki 2 baada ya dozi yako ya 2.




Je, ni SAWA kupata chanjo tofauti ya COVID-19 kwa dozi yangu ya 2?

Ndiyo! Ni salama na madhubuti katika kukuinga dhidi ya COVID-19 na aina zake.


Je, "uchanganyaji" wa chanjo ushawahi kufanywa hapo awali kwa chanjo zingine?

Ndiyo, ni jambo la kawaida sana. Kwa mfano, chapa tofauti za chanjo za homa ya manjano au surua mara nyingi huchanganywa.



Kwa nini ninapewa chanjo tofauti katika dozi ya 2?

Kuna uwezekano wa kupata chanjo tofauti nchini Canada katika wiki tofauti, na wakati mwingine chapa uliyopokea katika dozi ya 1 inaweza kukosekana kwa ajili ya dozi ya 2 wakati unapoweza kuipokea. Hatujui utasubiri kwa muda gani ili upate chanjo ya chapa sawa kwa ajili ya dozi ya 2. Kupata chanjo kwa ajili ya chanjo ya kwanza ya MRNA unayopewa (Moderna au Pfizer) ndiyo njia bora ya kujikinga na COVID-19.



Je, ni chanjo gani ya COVID-19 ninayopaswa kupokea katika dozi yangu ya pili?

Canada kwa sasa inatoa chanjo za COVID za Moderna na Pfizer kwa dozi nyingi za kwanza na za pili. Chanjo zote 2 zinafanana sana na zinafaa sana (ni fanisi karibu 95% katika kuzuia ugonjwa wa COVID baada ya dozi ya 2).

Ni salama kuchanganya aina tofauti za chanjo ya COVID-19 katika dozi zako za 1 na 2:



Chanjo Iliyopokelewa kwa ajili ya Dozi ya 1	Machaguo kwa ajili ya Dozi ya 2
Pfizer/BioNTech	Pfizer au Moderna Siku 21+ BAADA ya dozi ya 1
Moderna	Moderna au Pfizer Siku 28+ BAADA ya dozi ya 1
AstraZeneca	Pfizer au Moderna (inapendekezwa) au AstraZeneca Siku 56+ (wiki 8) BAADA ya dozi ya 1

Iwapo utatumia mchanganyiko wowote kati ya iliyopendekezwa, utakuwa umetimiza mahitaji ya chanjo kamili wiki 2 baada ya dozi ya 2.



Je, nitapata madhara tofauti ikiwa nitapata chanjo tofauti kwa dozi yangu ya 2?

Chanjo za COVID-19 za Moderna na Pfizer/BioNTech ni salama sana na zina madhara sawa. Madhara ya kawaida yanayoweza kutokea ni pamoja na maumivu ya sehemu ya bega/mkono uliodungwa sindano, maumivu ya mwili na misuli, baridi, kusikia uchovu na kuhisi homa. Watu wengine hupata madhara makubwa kidogo baada ya dozi yao ya pili ya chanjo (kwa mfano kuhisi uchovu zaidi au kuwa na maumivu makali zaidi ya misuli) - hii inamaanisha mfumo wako wa kinga unafanya kazi! Madhara haya kwa kawaida hupungua ndani ya siku moja hadi tatu.

Ni muhimu kwako kupokea dozi MBILI za chanjo za COVID-19 ili kutimiza mahitaji ya chanjo kamili dhidi ya COVID-19 na aina zake. Hii inakulinda wewe, wapendwa wako, na jamii yako dhidi ya ugonjwa wa COVID-19.



Tunatumani taarifa hii itakufaa! Tunakuomba usambaze taarifa hii kwa kiasi kikubwa, uitumie kama hati ya kurekodi faili la sauti au video, au kuitafsiri katika lugha zaidi ili kuisambaza kwa wengine. Tafadhali hakikisha umetaja chanzo: Women's College Hospital, OCASI, TAIBU Community Health Centre and Refugee 613.

Toleo hili linaanza kutumika Julai 7, 2021

Maelezo yaliyo katika taarifa hii yamethibitishwa na madaktari wa Canada: Meb Rashid MD, Profesa Msaidizi, Chuo Kikuu cha Toronto; Vanessa Redditt, MD, Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Toronto; na Isaac I. Bogoch, MD, Profesa Mshirika, Chuo Kikuu cha Toronto

Michango ya maudhui kutoka: Andrea Chittle, Kelly Grindrod, Noah Ivers, Samira Jeimy, Tara Kiran, Kate Miller, Menaka Pai, Adrian Poon, Samantha Yammine, Sabina Vohra-Miller, Kristen Watt, Holly Witteman



Funded by:



Immigration, Refugees and Citizenship Canada

Financé par :

Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada

With contributions from:

